بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHEMA NA MWENYE KUREHEMU

# Azimio la Waislamu Kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi Ulimwenguni

Nyota, jua na mwezi, na dunia hii, na vilivyomo vyote, wingi wake na ustawi wa jamii za viumbe mbali mbali vinavyoishi katika dunia, vinarejea kwake kuonesha shukrani zisizo na kikomo na rehma kwa muumba wao. Kimaumbile, vyote hivi vinamtumikia na kumuabudu na kumsujudia kwa utukufu wa Mola wao Mlezi. Sisi wanadamu tumeumbwa kumtumikia Mola wa viumbe vyote, kufanyia vizuri viumbe aina zote kwa kadiri tuwezavyo, ikiwa ni mmoja mmoja na ujumla wa vizazi vya viumbe alivyoviumba Allah

## TUNATHIBITISHA KUWA

### ALLAH NI MOLA MLEZI WA VIUMBE VYOTE:

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Shukrani zote zinamstahikia Allah Mola Mlezi wa viumbe vyote (Qur'an 1: 1)

هُوَ اللَّهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ

Ni yeye Allah, Muumbaji, Mtengenezaji wa Kila aina ya maumbile (Qur'an 59: 24)

الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهُ

Alieumba kila kitu kwa ukamilifu (Qur'an 32: 7)

### HAKUNA ALICHOKIUMBA PASINA KUWA NA UMUHIMU

Kila kitu kimeumwa kwa kupewa haki yake yaani kwa uthibitifu

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لَاعِبِينَ مَا خَلَقْنَاهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ

Na hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa ajili ya mchezo tu. Hatukuumba hivyo isipokuwa kwa haki na kuthibiti. (Qur'an 44: 38-39)

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُحِيطًا

Na vinamthibitikia yeye vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Allah amevizunguuka kuvijua vitu vyote. (Qur'an 4: 126)

وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ وَأَقِيمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ
وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ وَالْأَرْضَ وَضَعَهَا لِلْأَنَامِ

Allah amezinua kuziumba mbingu na ameweka kipimo. (mizaan)Ili msiharibu kipimo hicho Simamia katika kipimo kilichowekwa – Msichupe mipaka
Ameumba dunia kwa ajili ya viumbe vyote vinavyoishi (Qur'an 55: 7-10)

### UMBILE AU HALI ASILIA (FITRAH) ALIYOUMBA ALLAH

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَةَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ
ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

Elekea uso wako katika dini au imani iliyooka huo ni mfumo au maumbile halisia ambao Allah amewaum-bia watu
Hakuna mbadala kwa maumbile hayo ambayo Allah ameumba Ni njia iliyonyooka . Lakini watu wengi ha-waelewi (Qur'an 30: 30)

## TUNATAMBUA

UHARIBIFU (UFISADI) AMBAO MWANAADAM ANAUSABABISHA KATIKA ARDHI NI KUTOKANA NA MAHITAJI YA KIUCHUMI NA MATUMIZI YASIO NA KIKOMO

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

Umedhihiri uharibifu katika bara na bahari kutokana na yale yaliyofanywa na mikono ya watu; ili Allah apate kuwajaribu (kuwatahini)kutokana na baadhi ya yale waliyoyafanya, ili wapate kurejea kwa Allah (Qur'an 30: 41)

Mabdailiko ya tabia nchi ni matokeo ya matendo yetu ya uharibifu katika dunia. Sisi ni Miongoni mwa mkusanyiko wa viumbe hai tunaoishi pamoja na kuitumia hii. Ikiwa ni ni sehemu ndogo sana katika maamrisho ya kiiman, bado tuna uwezo wa kipekee ya kuchukua hatua ya kubeba jukumu la kuamrishana mema na kukatazana maovu kwa kadiri tuwezavyo.

لَخَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

Kwa yakini umbile la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbile la wanadamu lakini wengi Miongoni mwa watu hawatambui (Qur'an 40: 57)

وَمَا مِن دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُم

Na hakuna mnyama aliopo katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake ila ni umma (ja-mii) mfano wenu. (Qur'an 6: 38)

Hatuna haki ya kusababisha madhara au uharibifu dhidi ya viumbe wengine. Imani yetu inatuamrisha kuvichukulia viumbe vyote kwa hadhari sana katika hali ya kumuogopa Muumba wetu, Mwingi wa Re-hema na mwenye ihsani ya hali ya juu kwetu.

### TUNALAZIMIKA KUWAJIBIKA KWA MATENDO YETU

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

Basi, anaefanya wema hata wa uzito wa mdudu chungu ataona malipo yake; na anaefanya uovu hata uz-ito wa mdudu chungu nae ataona malipo yake. (Qur'an 99: 7-8)

## WITO WETU

Tunatoa wito kwa waislamu wote. Popote walipo kukabiliana na sababu za msingi za mabadiliko ya tabia nchi; uharibifu wa mazingira na kupotea kwa bio anuwai kwa kufata mfano wa Mtume wetu Muhammad ambae ameelezwa katika Quran "ni rehema kwa viumbe wote"
kwa kuzingatia maneno ya Mtume Muhammad (rehema na amani zimwendee Mtume Muhammad)
Dunia ni njema na ya yenye kijani kibichi, na kwa hakika amekufanya wewe kuwa msimamizi wa hiyodunia, na mnaangaliwa namna mnavyokuwa wacha Mungu kujitakasa katika jambo hilo.
(Hadīth ya Muslim kutoka kwa Abū Sa'īd Al-Khudrī)

ifees ecoislam

ISLAMIC RELIEF

Bango hili ni muhtasari wa Azimio la Waislamu kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyokubaliwa katika mkutano wa kimataifa wa mabadiliko ya tabia nchi uliofanyika Istambul uturuki mwezi wa Agosti mwaka 2015. Limetayarishwa kwa azma ya kushajiisha viongozi wa dunia wanaotoa maamuzi ambao wanakutana Paris Ufaransa Mwezi Disemba mwaka 2015 katika kikao cha 21 cha washirika wa mkutano wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia mabadiliko ya tabia nchi (COP 21).
Andika kamilifu lililotafsiriwa kwa lugha mbali mbali linapatika kupita tovuti ya www.ifees.org.uk

HASSEN RASOOL CREATIVE LABS